# HAKI ZA KIJAMII ZA VIJANA SHULENI

Swahili

## MAREJELEO


http://www.justice.gc.ca/eng/rp-pr/csj-sjc/jsp-sjp/rp02_8-dr02_8/p6.html

http://en.unesco.org/themes/women-s-and-girls-education

http://www.genderandeducation.com/resources-2/inclusion/promoting-gender-equality-in-schools/

http://www.theatlantic.com/education/archive/2014/03/the-never-ending-controversy-over-all-girls-education/284508/

https://blogs.unicef.org/evidence-for-action/migrant-children-face-higher-rates-of-bullying/

http://international.gc.ca/world-monde/aid-aide/child_soldiers-enfants_soldats.aspx?lang=eng

http://rightsofchildren.ca/wp-content/uploads/2016/01/CCRC-report-on-rights-of-children-in-Canada.pdf

https://www.bullyingcanada.ca/what-is-bullying

http://www.legalrightsforyouth.ca/rights-and-responsibilities/legal-responsibilities

http://www.legalrightsforyouth.ca/





SASKATCHEWAN SWIS COORDINATION
SSC

Funded by: Immigration, Refugees and Citizenship Canada

Financé par: Immigration, Réfugiés et Citoyenneté Canada

Brought to you by:
www.swissask.ca



## HAKI ZA KIJAMII ZA VIJANA SHULENI

Kuzoea mazingira ya shule nchini Canada kwaweza kuwa ngumu kwa vijana wanaoanza shule. Watoto na vijana hupitia shida shuleni kama kunyanyaswa na wenzao na migogoro mingine. Kwa wanafunzi wahamiaji na wakimbizi, shida zao hukiuka za wazaliwa wa Canada kwa sababu ya uzoefu na mazingira. Kuzoea jamii ya Marekani Kaskazini huchukua muda mrefu. Ni bora kwa shule zote kuwa na wakalimani na washauri wa kusaidia wanafunzi wapya kuzoea na kupata matokeo bora masomoni. Hata hivyo, jambo hili halifanyiki shuleni. Pia, kunaweza kuwa na mambo ya ukosefu wa usawa na ukosefu wa haki shuleni. Dhana ya haki yaweza kutofautiana katika nchi mbalimbali. Nchini Canada, haki za kijamii hujumuisha usawa na kukuza haki za kibanadamu kwa watu wote.



## USAWA WA KIKABILA

Canada ni nyumbani kwa watu wa kutoka kabila, tamaduni, jamii, na ukoo mbalimbali. Ni nchi yenye tamaduni zilizochanganyika na hujivunia tofauti hizi. Shule nchini zafaa kuiga mfano huu. Ubaguzi wa kikabila ni haramu na hukiuka Mkataba wa Haki na Uhuru wa Canada (Canadian Charter of Rights and Freedoms). Tangu kale, wachache kama watu wa kiasili na wahamiaji wamebaguliwa kikabila nchini Canada. Hata hivyo, ni muhimu kusitisha ubaguzi huu kupitia ushirikiano na jumuia. Ni muhimu kujivunia makabila mbalimbali na kuelewa kwamba tofauti hizi ni viungo vya utamaduni wa Canada.



# USAWA WA KIJINSIA

Shule za Canada ni sawa kwa wavulana na wasichana. Hakuna haja ya kuzitenganisha kwa sababu jinsia zote zina thamani sawa na zaweza kutangamana. Elimu ya pamoja yamaanisha kuwa vijana wote watapata fursa sawa usoni bila kubagua jinsia. Hili si jambo la Canada pekee ila ni la jamii zote ka kisasa duniani. Usawa wa kijinsia ni haki sawa kwa wanaume na wanawake, wasichana na wavulana. Kwa kuzingatia usawa huu, tamaduni zinazofaa zitadumishwa na zile nizazobagua kusitishwa.





# HAKI ZA WATOTO

Haki za watoto na vijana zimelindwa na sheria za Canada. Haki hizi ni kama:

- Uhuru kutokana na ukatili
- Uhuru kutokana na umaskini
- Uhuru kutokana na unyonyaji wa kazini na wa ngono
- Haki ya kuishi kwa afya na kupokea matibabu
- Haki ya masomo
- Haki ya kupokea ujumbe
- Haki ya kupokea ushauri wa kipekee kortini
- Haki ya kupokea huduma ya watoto na ukuzaji
- Haki ya kucheza
- Haki ya kujihusisha na familia, kujitambulisha, na utamaduni

Watoto wakimbizi na wahamiaji pia wana haki ya kuzingatiwa vyema na afisa wa uhamiaji kwa njia zinazofaa (Convention on the Rights of the Child / Mkataba wa Haki za Mtoto). Hivi, idara ya uhamiaji lazima izingatie kilicho bora kwa mtoto kabla ya kukata shauri. Mbali na hayo, vijana nchini Canada wana haki kama za watu wazima. Hizi ni kama vile haki ya kutochukuliwa hatia hadi kuthibitishwa na mahakama, haki ya kuhukumiwa kwa usawa, na haki ya kutopewa adhabu ya kikatili.

## UONEVU

Uonevu ni jambo la kawaida maishani ya watoto. Uonevu huhusisha tabia zozote zinazodhuru ama kuogofya mtoto shuleni. Tabia hizi sio za kimwili pekee. Uonevu unaweza pia kuwa kwa njia ya vitishio, matusi kulingana na maumbile, ukoo, kabila, mwelekeo wa kijinsia, mahali mtu atokako, na mengineyo. Kuwatenga watoto wengine, kusema uongo kuwahusu, kuwadhalilisha na kuwapiga ni baina ya uonevu mwingine.

Matokeo kwa alieonewa huwa mabaya kama kutojithamini, kuwa na mawazo ya kujiua, masuala ya afya ya akili, na kujitenga kwa aliyeonewa. Uonevu haukubaliwi kamwe.



## MAJUKUMU YA VIJANA KAMA RAIA WEMA

Kila mtu nchini Canada lazima afuate sheria hata kama hakubaliani nayo. Inasadikiwa kwamba kila mtu anajua sheria. Hii inawahusisha hata wenye mamlaka (kama serikali, jeshi, na polisi), na raia wa kawaida. Jinsi watu wote wanapopewa haki na uhuru nchini Canada, lazima pia wazingatie haki za watu wengine. Wasipofanya hivyo, wanaweza kupigwa faini au hata kuchukuliwa hatua ya kisheria.

Vijana wote kati ya miaka 12 hadi 17 wako chini ya Tendo la Haki ya Jinai ya Vijana (Youth Criminal Justice Act). Hii inamaanisha kwamba kijana anapovunja sheria anaweza hukumiwa na hakimu kwenye Korti La Jinai la Vijana. Kila mtu ana haki ya kuwakilishwa na mwanasheria na haki zake za kibinadamu kuzingatiwa.

